

SAUTI KUBWA

na Rangi Angavu

"Kwa nini Baba
wa Mbinguni
hafanyi makelele
makubwa yatoweke?"
Charlotte aliuliza.



NIELEZO NA ADAM HOWLING

Na Heather Sullivan
(Imetokana na hadithi ya kweli)

Hadithi hii iliteka huko Marekani.

Charlotte alichukia makelele! Hakupenda jinsi
Csauti zilivyopiga kwa nguvu katika masikio yake
au mwangwi kichwani. Hata alipojua kwamba yuko
salama, bado alihisi woga pale magari yalipotoa sauti
kali wakati yakifunga breki kwa ghafla na kwa nguvu.

Na Charlotte hakika hakupenda fataki!

Familia yake ilijaribu vitu vingi sana ili kumpa faraja
wakati palipokuwa na makelele. Baba alimnunulia
kiziba masikio maalumu ili kusaidia kuzuia kelele.
Kukiwa na radi, Mama alimkumbatia na kujificha
pamoja naye. Charlotte pia alisali kwa ajili ya kuomba
usaidizi ili asiogope.

Vitu hivi vyote vilisaidia. Lakini sauti kali bado
zilimfanya ahisi kuogopa.

"Tunakwenda kwenye maonyesho maalumu ya
fataki kwenye uwanja wa bustani usiku wa leo,"
Mama alimwambia Charlotte. "Je, unataka kuja?"

Charlotte alikunja uso. "Lakini fataki zina sauti kali."
"Sasa kwa vile wewe ni mkubwa, fataki inaweza
kuwa burudani kuangalia," Mama alisema. "Marafiki
zako wote watakuwa pale. Tunaweza kuleta vifaa
vyako maalumu vya kuziba masikio. Je, unadhani
utaweza kujaribu?"

Charlotte alishusha pumzi. "SAWA. Nadhani
ninaweza kujaribu."

Maonyesho ya fataki kwenye uwanja wa bustani
yalianza vizuri. Charlotte na marafiki zake walikimbia-
kimbia uwanjani kwenye nyasi, wakila vitafunwa na
kucheza michezo. Punde anga likawa giza. Charlotte
alikaa chini na kuvuta vifaa vyake maalumu vya
kuziba masikio akiangalia kwa woga angani.

BOOM! BOOM! PASUKA!

Charlotte moyo wake ulipiga kwa haraka zaidi, na
alihisi kifua chake kubana. Aliruka juu na alijaribu
kukimbia mbali na yale mabomu yaliyomzunguka.

Mama alimkimbilia Charlotte na kumkamata.
Walirudi na kukaa chini, na Mama akamkumbatia
kwa karibu. Machozi yalianguka usoni mwa Charlotte.

"Nasikitika hilo limekuogopesha wewe," Mama
alisema. "Niko hapa tu. Acha tufokasi juu ya rangi ili
usisikie sauti zaidi. Unaona nini kwa macho yako?"

Charlotte alivuta pumzi kubwa. "Naona dhahabu,
na nyekundu, na kijani."

"Sasa tumia pua yako," Mama alisema. "Unavuta
harufu gani?"

"Ninaweza kuhisi harufu ya moshi na nyasi,"
alisema Charlotte. "Na bisi!"

"Ni hisia gani nyingine unaweza kutumia sasa hivi?"

Charlotte alifumba macho yake. "Ninaweza
kuhisi. Fataki zinapolipuka, ninaweza kuhisi kifua
changu kinatikisika."

"Je, unaweza kuonja kitu chochote?" Mama aliuliza.

Charlotte alitoa ulimi wake nje. "Siwezi kuonja hizi
fataki." Alicheka.

Vyote hivi vilimfanya Charlotte kuwa na hamu ya
kujuu. *Watu wanazifanyaje hizi rangi tofauti?* Alijuiliza
kwa mshangao. *Kwa nini fataki zinalipuka? Je, ni
kwa jinsi gani zinatengeneza maumbo tofauti?* Fataki
hazikuonekana kutisha tena sasa.

"Mama, fataki ni za kushangaza!" Charlotte alisema.

Mama alipokuwa akimlaza Charlotte kitandani
usiku ule, Charlotte aliuliza, "Kwa nini Baba wa
Mbinguni hajajibu sala zangu nilipomwomba
kuyaondolea mbali makelele?"

Mama aliwaza kwa muda. "Baba wa Mbinguni
siyo daima atayaondoa mbali mambo yanayotisha,"
alisema. Lakini wakati mwingine Yeye anatusaidia sis
kuona mambo katika njia tofauti au kutupatia watu
wanaosaidia kutufariji."

"Kama vile aliyyonisaidia mimi usiku wa leo!"
alisema Charlotte

"Hiyo ni sawa!" Mama alitabasamu. "Ulienda
kwenye onyesho la fataki licha ya kuwa unaogopa.
Ndipo Baba wa Mbinguni amekusaidia kutuliza hofu
yako. Yeye pia amekusaidia kuona uzuri wa fataki
kwa kutumia milango yako mingine ya fahamu.

Charlotte alifikiria juu ya rangi angavu katika anga
na kutabasamu. Bado hakutaka sauti kubwa. Bado
zilimwogopesha lakini aliju Baba wa Mbinguni
daima angeweza kumsaidia kuwa jasiri. ●

"Usiogope; kwani Mimi niko
pamoja nawe" (Isaya 41:10).